

JAMHURI YA MUUNGANO WA TANZANIA
OFISI YA RAIS
TAWALA ZA MIKOA NA SERIKALI ZA MITAA



MTIHANI WA UTAMILIFU (MOCK) KIDATO CHA NNE
KANDA YA ZIWA
(GEITA, KAGERA, MARA, SIMIYU, SHINYANGA NA MWANZA)

021

KISWAHILI

(Kwa Watahiniwa wote wa Shule na Kujitegemea)

Muda: Saa 3

Mwaka: 2025

MAELEKEZO

1. Mtihani huu una jumla ya sehemu A, B na C zenye jumla ya **maswali 11**.
2. Jibu maswali **yote** katika sehemu A na B na chagua maswali **mawili** kutoka sehemu C.
3. Andika namba yako ya mtihani kwa kila karatasi yako ya kujibia.
4. Zingatia maagizo ya kila sehemu na ya kila swali.
5. Swali la tisa (9) ni **la lazima**.

SEHEMU A: (ALAMA 16)

Jibu maswali yote kutoka sehemu hii.

1. (i) "**Bumbura** *[bu'mbura/ nm (.) [a-/wa.]* Samaki wa maji chumvi mwenye macho manne anayefanana na chewa au mzia lakini mfupi." Hii ni sehemu ya kamusi. Kifungu cha maneno kilichopigiwa mstari katika dhana ya kamusi huitwaje?
A. Homonimu B. Kidakizo
C. Kitomeo D. Etimolojia ya neon ()
E. Matamshi ya neno
- (ii) Katika harakati za kuimalisha sekta ya viwanda, serikali ya Tanzania imekuwa ikiagiza "Mashine" kutoka nchi za nje. Neno "Mashine" limeundwa kwa mbinu gani katika lugha Kiswahili.
A. Ukopaji B. Ufupishaji
C. Uradidi D. Ufananisho wa sauti ()
E. Uthoaji

6. (a) Mnamo mwaka 2009, Idara ya Kiswahili na Tuki ziliungana kuunda taasisi inayoitwa TATAKI. Eleza majukumu manne ya asasi hiyo.
- (b) Kwa kutumia mfano, toa maana ya istilahi zifuatavyo kama zinavyotunika katika lugha ya Kiswahili.
 - (i) Pijini
 - (ii) Kamusi
 - (iii) Lahaja
7. Suala la mapenzi lisipochukuliwa kwa tahadhari linaweza kusababisha madhara mengi katika jamii. Thibitisha ukweli wa kauli hiyo kwa kutoa hoja sita kutoka katika tamthiliya ya orodha.
8. Soma shairi lifuatalo kisha ujibu maswali yanayofuata.

Titi la mama ni tamu, hata likawa la mbwa,
 Kiswahili adhimu, sifayo iliyofumbwa,
 Kwa wasio kifahamu, niimbe ilivyo kubwa,
 Titile mama li tamu, jingine haliishi hamu,
 Lugha yangu ya utoto, hata sasa nimekuwa,
 Tangu ulimi mzito, sasa kusema najua,
 Ni sawa na manukato, moyoni mwangu na pua,
 Titile mama li tamu, jingine haliishi hamu.

Maswali

- (a) Pendekeza kichwa cha shairi kisichozidi maneno matatu.
- (b) Neno “Titile” limetumia kunga ya kufupisha maneno katika ushairi ili kupata ulinganifu wa mizani. Taja dhana hiyo.
- (c) Taja silabi za ndani na nje katika ubeti wa pili.
- (d) Mapigo ya kimuziki yanayolifanya shairi hilo liimbike ambayo hupimwa kwa idadi ya silabi huitwa?.
- (e) Kutokana na shairi ulilosoma, ujumbe gani umeupata.

SEHEMU C: (ALAMA 30)

Jibu maswali mawili kutoka sehemu hii. Swali la tisa ni **la lazima**

9. “Baada ya 1961 hadi leo waandishi wengi wa fasihi nchini Tanzania wamejikita katika kuhakikisha upatikanaji wa usawa, haki na ustawi wa watu kwa ujumla”. Kwa kutumia diwani mbili ulizosoma, fafania namna walivyofanikiwa kutekeleza wajibu wao wa ujenzi wa jamii mpya. Toa hoja tatu kwa kila kitabu.
10. Lugha inapotumiwa vizuri katika kazi za fasihi hurahisisha kufikisha ujumbe wake kwa jamii iliyokusudiwa. Tumia vipengele vitatu vya tamathali za semi kuthibitisha kauli hiyo kutoka katika kila kitabu kati ya riwaya mbili ulizosoma.
11. Msanii wa kazi ya fasihi hubuni na kutumia mandhari vizuri ili yamsaidie kufikisha alichokusudia katika jamii. Thibitisha ukweli wa kauli hiyo kwa kutumia tamthiliya mbili ulizosoma. Toa hoja tatu kwa kila kitabu.